

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam
Tarehe 7 Julai 2007**

Waliohuduria

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishekh
Ally Salum
Bakari Sadiki
Elaine Baker
Emmy Rashidy
Filbert Mbecha
Godfrey Jax (CHABADA)
Hamadi H Bwaja
Ima Mhigai
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kilenja Kasim Ramadhan
Lameck Charles
Paulo Atibu Hatibu
Rajabu S Mkialiko
Said Mangala
Saidi Mbaruku
Sudi Saidi

Msafara wa Baiskeli

Mkutano ulimkaribisha Godfrey jax ambaye ni mwanachama wa CHABADA, shirika linalojihusisha na baiskeli kama michezo. Alijiunga pia na UWABA. Ilikubalika kuwa kamati iundwe kwa ajili ya msafara ikiwa na wajumbe watatu kwa kila shirika (UWABA, CHABADA na AALCOM) Godfrey alisema kuwa yeye atakuwa miongoni mwa wajumbe toka CHABADA pamoja na kengele, na Hussein Ali. Waumbe wa UWABA watakuwa Ali Juma Jongo, Ally Saidi Mohammedi na Elaine Baker. Godfrey alikubali kuwasiliana na AALCOM ili kupata washiriki. Ilikubalika kuwa kamati hii maalumu itakutana wiki ijayo jumamosi saa tatu asubuhi pale Mahakama ya Ndizi Mabibo, kabla ya mkutano rasmi wa UWABA ikiwa itakuwa sawa kwa AALOCOM.

Akaunti Benki

Ally Saidi aliarifu kuwa aliongea na mwenyekiti wa mtaa wa jitegemee (Rashid Chikoyo), sehemu mikutano yetu inapofanyika alikubali kutambulisha ili tufungue akaunti. Elaine alinipa Ally Saidi Mohamed barua ya UWABA kwenda NMB, nakala ya katiba na nakala ya dondoo za mkutano tulioamka kufungua akaunti benki, picha za pasipoti za mejah, Elaine na Juma. Ally Saidi Mohammedi alisema atapeleka nyaraka hizo kwa mwenyekiti wa mtaa ili picha zipigwe mhuri na kuchukua barua ya utambuzi.

Ofisi

Elaine aliarifu kuwa ametuma barua pepe kwenye mashirika mbalimbali ulimwenguni kuomba msaada wa kifedha kwa ofisi yetu, mawili kati ya hayo yalijibu wakisema kuwa hawana fedha. Alisema kuwa mwanachama wa UWABA Joey lake ameahidi kuchangia Tsh 50,000. wanachama wengine walitoa mchango Tsh 10,500 na zilirekodiwa kwenye kitabu cha akaunti cha Juma.

Mpango madhubuti wa Usafiri Dar es Salaam

Juma alituarifu kuwa alipeleka barua ya kushiriki kwetu kwenye mpango madhubuti wa usafiri Dar es Salaam kwenye halmashauri ya jiji, JICA na Taasisi ya usafirishaji Dar es Salaam.

Anauani ya Posta

Tunatumia sanduku la barua la Mejah kwa masuala ya UWABA. Ilionekana kuwa ni muhimu kuwa na nakala ya ufunguo kwa ajili ya UWABA kwani tutaweza kupata majibu ya barua zetu bila kujua. Elaine na Juma walisema watafuatilia.

Barabara zilizo kwenye mpango wa ujenzi.

Elaine alijaribu kupiga simu na kutuma ujumbe kwa Carl Bro Associates ila hakufanikiwa kuwapata atajaribu kuwatumia barua pepe wiki hii.

Mengineyo

Wanachama zaidi walichukua vitambulisho na kuchanga Tsh 500 kwa ajili ya gharama. Jumanne alihifadhi michango.

Godfrey Jax alisema CHABADA wamepanga kufanya mashindano ya maguta kutoka TAZARA hadi uwanja wa ndege kasha kurudi TAZARA, toka kibaha na kurudi TAZARA. Wanatarajia kuwa na guta jipya kama zawadi kwa mshindi kisha atatufahamisha mapema.